**21-Iltiqaaul-Harfaynis-Saakinayni (Mkutano Wa Herufi Mbili Za Saakinah)**

**إِلْتِقَآءُ الْحَرْفَيْنِ السَّاكِنَيْنِ**

**إِلْتِقَآءُ الْحَرْفَيْنِ السَّاكِنَيْنِ Iltiqaaul-Harfaynis-Saakinayni - Mkutano wa herufi mbili zenye sukuwn:**

Katika lugha ya Kiarabu, Waarabu hawakusanyi baina ya sukuwn mbili. Kukutana kwa sukuwn mbili inatokea ima katika neno moja au katika maneno mawili. Hivyo basi zinapokutana herufi mbili na zote zikawa ni zenye sukuwn hutekelezwa hukmu zake ili kuwepesisha kutamkwa. Kukutana huko kwa sukuwn mbili hutokea kwa sababu zifuatazo:

1. **Kukutana sukuwn mbili katika neno moja:**

i) Zinapokutana herufi mbili zenye sukuwn mojawapo ikawa ni herufi ya مَدّ (ا ي و) na kabla yake kuna *i'raab*, au مَدُّ اللّين (و ي) saakinah na kabla yake kuna *i'raab* ya fat-hah[1]

<table>
<tr><th colspan="2">Kuweko Madd; ا و ي</th></tr>
<tr><td>Hapa kuna mifano miwili ya kukutana kwa sukuwn mbilii:<br>i) imekutana herufi ya madd آ katika (حآ) na ج yenye shaddah kwa sababu asili ya shaddah ni herufi mbili; moja ina sukuwn na moja ina i'raab..<br><br>ii) Imekutana tena herufi ya madd و ambayo ni saakin na ن yenye shaddah;</td><td>أَتُحَآجُّوٓنِّى<br><br><br><br><br>ٱلصَّآخَّةُ</td></tr>
</table>

[1] Rejea mlango wa 'Maddut-twabiy'iy – maddul-liyn'

| | |
|---|---|
| Imekutana herufi ya madd آ ambayo ni saakin na herufi ya خ yenye shaddah.<br>Kukutana kwa herufi ya madd و yenye sukuwn na ن yenye sukuwn ya asili.<br><br>Kukutana kwa herufi madd ya ي yenye sukuwn na ن yenye sukuwn ya asili. | نٓ (نون)<br><br>يسٓ (ياسين) |
| **Kuweko مَدُّ اللّين (Maddul-Liyn)** | |
| Kukutana kwa herufi ya ي saakinah na ن saakinah ya asili katika kutamka huruwuf hizo za al-muqatwtwa'ah | عَيْن (عٓسٓق) |

ii) Inapokuwa herufi ya pili imekuwa na sukuwn ingawa asili yake ilikuwa na *i'raab*, lakini kwa sababu ya kusimama imesababisha kuwa na sukuwn.

| **Inapokuwa herufi ya pili ni ya kusimamiwa** | |
|---|---|
| Imekutana herufi ya madd ا و ي saakinah na herufi za mwisho ن و ب ambazo zilikuwa na *i'raab* lakini zimepewa sukuwn kwa sababu ya kusimamia.<br><br>Imekutana herufi ya mwisho iliyokuwa na *i'raab* lakini imepewa sukuwn kwa sababu ya kusimamia pamoja na herufi saakin iliyo kabla yake.<br><br>Kukutana kwa herufi ya mwisho iliyokuwa na *i'raab* lakini imepewa sukuwn kwa sababu ya kusimamia na | رَبِّ الْعَالَمِينْ<br>شَكُورْ<br>الْعِقَابْ<br>والْفَجْرْ – والْعَصْرْ – لَفِي خُسْرْ<br><br>قُرَيْشْ – مِنْ خَوْفْ |

| | |
|---|---|
| herufi ya kabla yake ambayo ya al-liyn yenye sukuwn. | |

2. **Mkutano wa sukuwn mbili katika maneno mawili:**

Inapokuwa neno la mwanzo limemalizikia na herufi saakin na neno la pili likawa na sukuwn hapana budi isipokuwa hukmu mbili zifuatazo:

- Zinapokutana sukuwn mbili ya mwanzo ikawa herufi ya madd ا و ي wakati huo hudondoka herufi ya madd katika kutamkwa na huthibiti kimandishi.

- Zinapokutana sukuwn mbili ya mwanzo ikawa sio katika herufi za madd; hutiwa *i'raab* hiyo herufi ya mwanzo kutegemea na neno.

**i) Kudondoka herufi ya mwanzo inapokuwa imefuatiwa na madd:**

| Badala ya kutamkwa | Hutakiwa kutamkwa | Mifano |
|---|---|---|
| **wa idh QaaluwAllaahumma** | **wa idh qaalu-LLaahumma** | وَإِذۡ قَالُواْ ٱللَّهُمَّ |
| **afiy Allaahi ..** | **afi-LLaahi ..** | أَفِي ٱللَّهِ شَكٌّ |
| **wa qaalaa Al-HamduliLLaahi** | **wa qaalal-Hamduli-LLaahi** | وَقَالَا ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ |
| **Idhaa as-samaaaaau ..** | **Idhas-samaaaaau…** | إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنفَطَرَتۡ |

ii) Kutiwa *i'raab* herufi ya mwanzo kutegemea na neno.

Kutiwa fat-hah:

| Sababu | Badala Ya Kutamkwa | Hutakiwa Kutamkwa | Mifano |
|---|---|---|---|
| Neno مِنْ asili yake lina sukuwn | **... min Allaahi ...** | **... mina-LLaahi ...** | فَلَمۡ يُغۡنِيَا عَنۡهُمَا مِنَ ٱللَّهِ شَيۡـًٔا |
| | **... min al-khaasiryn** | **... minal-khaasiryn...** | فَأَصۡبَحۡتُم مِّنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ |
| Herufi ya ي ni ya 'al-Mutakallim' (msemaji) ambayo asli yake huwa na sukuwn | **...Ni'matiy allatiy ...** | **... Ni'matiya-llaatiy ...** | ٱذۡكُرُواْ نِعۡمَتِيَ ٱلَّتِيٓ أَنۡعَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ |

Kutiwa kasrah:

| Sababu | Badala ya kutamkwa | Hutakiwa kutamkwa | Mifano |
|---|---|---|---|
| Kumalizikia sukuwn ya Tanwiyn katika neno la qawman | **qawman Allaahu** | **qawmani-LLaahu**<br><br>**Bonyeza usikilize** | لِمَ تَعِظُونَ قَوْمًا ٱللَّهُ ۙ [2] |
| Kumalizikia sukuwna ya Tanwiyn katika neno la jazaaaan | **jazaaaan al-husnaa** | **...jazaaaaanil-husnaa**<br><br>**Bonyeza usikilize** | فَلَهُۥ جَزَآءً ٱلْحُسْنَىٰ [3] |
| Kumalizikia sukuwn ya Tanwiyn katika neno la yawmaidhin | **yawmaidhin al-mustaqarr** | **...yawmaidhinil-mustaqarr**<br><br>**Bonyeza usikilize** | إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ ٱلْمُسْتَقَرُّ [4] |
| Kumalizikia sukuwna ya Tanwiyn katika neno la rahbaaniyyatan | **wa rahbaaniyyah ibtada'uwhaa** | **wa rahbaaniyyatanib-tada'uwhaa**<br><br>**Bonyeza usikilize** | وَرَهْبَانِيَّةً ٱبْتَدَعُوهَا [5] |
| Kumalizikia na sukuwn katika herufi ya ي ambayo ni yaa ya 'al- | **yaa swaahibayy as-sijni** | **yaa swaahibayyis-sijni**<br><br>**Bonyeza usikilize** | يَٰصَٰحِبَيِ ٱلسِّجْنِ [6] |

[2] Al-A'raaf (7: 164)
[3] Al-Kahf (18: 88)
[4] Al-Qiyaamah (75: 12)
[5] Al-Hadiyd (57: 27)
[6] Yuwsuf (12: 39)

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mutakallim' (msemaji) ambayo asli yake huwa na sukuwn | | | |

Kutiwa dhwammah:

| Sababu | Badala ya kutamkwa | Hutakiwa kutamkwa | Mifano |
|---|---|---|---|
| Neno la mwanzo linamalizikia na herufi za وا kuonyesha wingi ambayo inamalizika na sukuwn | **da'awuw Allaah** | **da'awu-LLaaha** | دَعَوُاْ ٱللَّهَ |
| | **wa 'aswawuw ar-Rasuwla** | **wa 'aswawur-Rasuwla** | وَعَصَوُاْ ٱلرَّسُولَ |
| Neno yamassuhum (wingi) asili yake linamalizika na sukuwn | **laa yamassuhum as-suw-u** | **laa yamassuhumus -suw-u** | لَا يَمَسُّهُمُ ٱلسُّوٓءُ |
| Neno 'alaykum (wingi) asili yake linamalizikia na sukuwn | **'alaykum al-qitaalu** | **'alaykumul-qitaalu** | عَلَيۡكُمُ ٱلۡقِتَالُ |